

# Bibilia ya watoto

## Inaleta

### Pasaka ya kwanza



Kimeandikwa na: Edward Hughes  
Kimeorodheshwa na: Janie Forest; Alastair P.  
Imerekebishwa na: Lyn Doerksen  
Kimetafsiriwa na: Grace Chepkoech  
Kimedhibitishwa na: Bible for Children  
[www.M1914.org](http://www.M1914.org)

BFC  
PO Box 3  
Winnipeg, MB R3C 2G1  
Canada

©2026 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.



Mwanamke alisimama chini ya mlima  
palipokuwa na makelele, macho yake  
yenye huzuni yakitazamia  
ambapo palikuwa na  
jambo la kuhuzunisha.  
Mwana wake alikuwa  
anakufa. Mwanamke  
huyu alikuwa Maria,  
na alisimama mahali  
ambapo Yesu  
alikuwa  
amesulubishwa  
msalabani.





Haya yote yalitendekaje?  
Maisha ya Yesu ya  
kupendeza yangeishaje  
katika njia hii ya  
kutisha? Mungu  
alikutubalia aje  
mwana wake  
asulubishwe  
msalabani hadi afe pale?  
Yesu alifanya kosa kuhusu  
yeye ni nani? Kweli Mungu  
alikosea pale?






La! Mungu hakukosea.  
Yesu hakuwa amefanya  
kosa lolote. Yesu  
alikuwa anajua kuwa  
atauliwa na watu waovu.  
Hata Yesu alipokuwa  
mtoto mchanga, mzee  
mmoja aitwaye Simioni  
alimwambia Maria kuwa  
wangepatwa na huzuni  
hapo mbele.



Siku chache  
kabla Yesu auawe,  
mwanamke mmoja alikuja  
na kumwaga manukato  
miguuni mwa Yesu.

"Huyu anapoteza pesa  
bure," wanafunzi wa Yesu  
walilalamika. "Ametenda jambo  
njema," Yesu akasema. "Amelitenda  
kwa kuzikwa kwangu. Maneno ya kutisha haya!



Baada ya haya, Yuda  
Iskariote, mwanafunzi  
mmojakati ya kumi na  
wawili wa Yesu, alikubali  
kumsaliti Yesu kwa kuhani  
mkuu ili apate fedha 30.



Katika sikukuu ya wayahudi ya pasaka, Yesu alikula chakula chake cha mwisho pamoja na wanafunzi wake. Aliwaelezea maneno makuu kumhusu Mungu na ahadi zake kwa wale wanaompenda. Halafu Yesu akawapa mkate na kikombe wagawane. Haya yalikuwa ya

kuwakumbusha kuwa mwili na damu ya Yesu tulipewa ili kuleta msamaha wa dhambi.



Hapo Yesu akawaambia marafiki wake kuwa atasalitiwa na wao watatoroka. "Mimi sitatoroka," Petero akasema. "Kabla jogoo hajawika leo, utanikana mara tatu," Yesu akasema.






Baadaye usiku huo,  
Yesu alikwenda  
kuomba katika  
bustani Gethsemani.  
Wanafunzi wake  
waliokuwa naye  
wakasinzia. "Ee  
Baba," Yesu aliomba,  
"... uniondolee  
kikombe hiki.  
Walakini si mapenzi  
yangu bali yako  
itendeke."



Muda si muda kikundi cha watu wakaingia bustani mle, wakiwa wanaongozwa na Yuda. Yesu hakukataa, lakini Petro akakata sikio la mtu. Kimya, Yesu akamgusa sikio na kumponya. Yesu alijua kukamatwa kwake kulikuwa ni mapenzi ya Mungu.




Kikundi kile kilimchukua Yesu kwenye nyumba la kuhani mkuu. Pale, viongozi wa wayahudi wakasema kuwa Yesu lazima afe. Hapo karibu, Petero alikuwa anasimama karibu na moto la wafanyakazi akitazama.




Mara tatu watu walimtaja Petero na kusema,  
"Wewe ulikuwa na Yesu!" Mara tatu Petero alikana,  
kama vile Yesu  
alisema atafanya.  
Petero hata  
alitukana.



Hapo, jogoo akawika.  
Ilikuwa ni kama sauti  
ya Mungu kwa Petero.  
Akikumbuka maneno  
ya Yesu, Petero  
akalia kwa majonzi.





Yuda alisikia vibaya pia. Alijua kuwa Yesu hakuwa ametenda chochote kibaya. Yuda alirudisha fedha ile thelathini lakini makuhani walikataa kuichukua. Yuda alitupa fedha ile chini, akaenda nje na kujinyonga.






Makuhani wakamleta  
Yesu mbele ya Pilato,  
mkubwa wa Warumi.  
Pilato akasema,  
“Sijapata kosa lolote  
na mtu huyu.” Lakini  
watu wakazidi kusema,  
“Asulubishwe!  
Asulubishwe!”



Mwishowe Pilato akakubali  
na kumhukumu Yesu kifo  
msalabani. Askari walimpiga  
Yesu na kumtemea mate  
usoni, na kumcharaza viboko.  
Walimtengenezea taji la  
miiba na kumvisha kichwani.  
Halafu wakamsulubisha  
msalabani kwa  
misumari ili afe.



Yesu alikuwa amejua tayari kuwa angekufa vile. Alijua pia kuwa kifo chake kingeleta msamaha wa dhambi kwa wale wamwaminio. Wahalifu wawili


walisulubishwa kando yake.

Mmoja alimwamini

Yesu - na alienda paradiso. Yule

mwingine


hakumwamini.



Baada ya masaa ya kuteseka,  
Yesu akasema, "Imekwisha"  
na akafa. Kazi yake  
ilikuwa imeisha.  
Marafiki wake  
walimzika  
katika kaburi  
lililochongwa  
mwambani.



Halafu askari wa  
Warumi wakafunga  
na kulichunga kaburi.  
Sasa hakuna  
ambaye angeingia  
wala kutoka pale.



Kama hii ingekuwa mwisho  
wa hadithi, ingekuwa ya  
kuhuzunisha. Lakini  
Mungu akatenda  
jambo la ajabu.  
Yesu hakubaki  
kifoni!




Asubuhi na mapema ya siku  
ya kwanza katika wiki,  
wanafunzi wachache  
wa Yesu walipata  
jiwe limeondolewa  
kaburini.

Walipoangalia  
ndani, Yesu  
hakuwa pale.



Mwanamke mmoja akabakia  
akilia. Yesu alimtokezea!  
Alikimbia na kuenda  
kuwaelezea wengine kwa  
furaha. "YESU YU HAI!  
YESU AMEFUFUKA  
KIFONI!"





---

Punde Yesu akaja walipokuwa wanafunzi wake na kuwaonyesha alama mikononi ya msumari. Ilikuwa kweli. **YESU ALIKUWA HAI TENA!** Alimsamehe Petero kwa kumkana, na akawaambia wanafunzi wawaeleze kila mtu kumhusu yeye. Halafu akarudi mbinguni alipotoka hiyo siku ya krismasi ya kwanza.



# Pasaka ya kwanza

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,


inapatikana katika

Matayo 26-28, Luka 22-24, Yohana 13-21

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."


Zaburi 119:130





Mwisho

54



60



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

